Nambari ya Mtahiniwa ___________________

SMZ

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA DARASA LA NNE

121 KISWAHILI

MUDA: SAA 2.00 JUMATATU 14 DISEMBA, 2020 MCHANA

---

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C na D.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A na B. Swali MOJA (1) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu YOTE yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Majibu YOTE yaandikwe kwa kalamu ya buluu au nyeusi.
6. Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.

| KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI | | |
|---|---|---|
| NAMBARI YA SWALI | ALAMA | SAINI |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |
| JUMLA | | |

Mtihani huu una kurasa 12 zenye maandishi



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Nambari ya Mtahiniwa ___________________

SEHEMU A: (Alama 20)

UFAHAMU

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

1. Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.

Kijana anahitaji kuwa na rafiki ili aweze kuondokana na <u>upweke</u> pamoja na kupata <u>faraja</u>. Aidha, hali hiyo itajitokeza kwa sababu atafahamiana na marafiki hao. Vilevile atazoeana nao hasa kwa kupitia mazungumzo. Kijana anaweza kupata marafiki popote pale. Kwa mfano; skuli, kazini, sehemu za ibada, safarini na hata miongoni mwa majirani zake.

Lakini kijana anapaswa kuwa mwangalifu sana katika kuchagua marafiki. Katika makuzi yake, kijana huwa karibu sana na rafiki zake. Marafiki kwa kiasi kikubwa huwa na nguvu za <u>kuambukizana</u> tabia nzuri au mbaya. Kwa hivyo ni jukumu la wazazi kumuelekeza na kumshauri kijana kutafuta rafiki mwema. Ni kheri kukosa rafiki kuliko kuwa na rafiki mlevi, muongo, mwizi, mvivu, mchafu au mtumiaji wa dawa za kulevya. Rafiki mzuri ni yule mwenye tabia njema na busara, ambaye hutoa <u>ushauri</u> mzuri unaoweza kumsaidia mtu kupata mafanikio katika maisha.

Maswali

a) Kuna umuhimu gani wa kijana kuwa na rafiki?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

b) Taja maeneo manne (4) ambayo kijana anaweza kupata marafiki.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

c) Kwa nini kijana anapaswa kuwa mwangalifu katika kuchagua marafiki?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

d) Eleza jukumu la wazazi kwa kijana katika kuchagua rafiki.

_______________________________________________

_______________________________________________

e) Taja sifa mbili (2) za rafiki mwema.

i. _______________________________________________

_______________________________________________

ii. _______________________________________________

_______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

2. Tunga sentensi kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mstari katika habari uliyoisoma hapo juu.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU B: (Alama 40)

## SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

3. Andika mfano mmoja (1) kwa kila nomino ya pekee iliyopo katika jadweli lifuatalo.
Nambari moja (i) imetumika kama mfano.

| NOMINO YA PEKEE | | MFANO |
|---|---|---|
| i. | Nomino ya mahali | Zanzibar |
| ii. | Nomino ya mlima | |
| iii. | Nomino ya mwezi | |
| iv. | Nomino ya mtu binafsi | |
| v. | Nomino ya siku | |
| vi. | Nomino ya mto | |



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

4. a) Bainisha wakati uliotumika katika sentensi zifuatazo.

Nambari moja (i) imetumika kama mfano.

i. Mwalimu atakuja kesho.
Wakati ujao_______________________________

ii. Mgonjwa aliyelazwa hospitali ameruhusiwa.

_______________________________

iii. Wageni hawatosafiri kwa boti wala ndege.

_______________________________

vi. Watu wengi hawapendi kuchunguza afya zao.

_______________________________

b) Tunga sentensi zenye aina zifuatazo za maneno.

i. Kitenzi kishirikishi

_______________________________

_______________________________

ii. Kiwakilishi cha pekee

_______________________________

_______________________________

5. a) Andika maneno yafuatayo kwa nambari.

i. Elfu kumi na tano mia mbili na sita.

_______________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

ii. Laki moja na kumi.

______________________________________________

iii. Laki nne, elfu thelathini na tatu na thelathini na tatu.

______________________________________________

b) Andika nambari zifuatazo kwa maneno.

i. 6,909

______________________________________________

______________________________________________

ii. 203,000

______________________________________________

______________________________________________

6. a) Tafsiri aya ifuatayo kwa Kiswahili.

My grandfather goes to the market every morning. When he gets there, he buys some fruits such as pineapples, water melons, avocados and guavas. He also buys vegetables, onions and meat. He buys some spices too.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

b) i. Nini maana ya kongamano?

ii. Eleza faida mbili (2) za kongamano.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Nambari ya Mtahiniwa ____________________

SEHEMU C: (Alama 20)

FASIHI

Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii.

7. Buni hadithi fupi kutokana na picha ifuatayo.



______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

8. a) i. Nini maana ya riwaya?

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

ii. Taja jina jengine la riwaya.

_______________________________________________

_______________________________________________

iii. Andika sababu inayopelekea masimulizi ya kawaida kutofautiana na masimulizi ya hadithi.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

b) Eleza maana ya nahau zifuatazo.

i. Kufyata mkia

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

ii. Kutia chumvi

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Nambari ya Mtahiniwa ____________________

## SEHEMU D: (Alama 20)

## UTUNGAJI

Jibu swali MOJA (1) tu katika sehemu hii.

9. Ifuatayo ni barua ya kawaida ambayo haiko katika mpangilio sahihi, ipange barua hiyo kwa usahihi kwa kutumia herufi zilizomo katika kila kipengele. Kipengele cha kwanza kimetumika kama mfano katika jadweli lililopo chini ya barua.

Baba mpendwa, } A

Wako Mwanao,
Sikuzani Mambo. } B

Madhumuni ya barua hii ni kukujulisha kuwa, pesa ulizonitumia zimenifika. Nakushukuru sana baba. } C

Skuli ya Msingi Mtakuja,
S.L.P 991,
Miti Ulaya, Zanzibar.
20/12/2020. } D

Nisalimie sana mama na wote wanaonifahamu hapo mtaani. } E

Shikamoo baba. Natumai kuwa wewe ni mzima pamoja na mama na ndugu zangu wote. Mimi mzima pia. } F

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
|---|---|---|---|---|---|
| D | | | | | |



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

10. Eleza tofauti tano (5) kati ya kadi ya mwaliko na barua ya simu.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org